**Kampeni ya Kuamsha Waislamu Dhidi ya Ahmadiyya,**

**Juni 30, 1996**

# Bismillahir Rahmanir Rahim

***Mapenzi ya Allah pamoja na Rehema Zake ziwe juu ya Sayidina Muhammad na Ahli zake, na Maswahaba wake.***

**Mtume Muhammad (saw) anasema:**

**'KILA ULEVI NI HARAMU'**

**(Muslim, Al-Mawatta & Abu Dawuud)**

## DAWA ZA KULEVYA NA JUMUIYA YA AHMADIYYA

(Na Dkt. Sayd Rashid Ali)

Matumizi ya dawa za kulevya na ulevi ni tatizo la dunia nzima, tatizo hili limezidi kuwa kubwa katika miaka ya karibuni hasahasa miongoni mwa vijana. Hili ndilo tatizo linalolalamikiwa kusababisha kiwango kikubwa cha uhalifu na fujo, ndilo kiini cha kusambaratika kwa familia, na ndilo linalowashughulisha, kwa kiasi kikubwa, viongozi, watumishi wa kada za kijamii, Polisi pamoja na walimu na madaktari. Unga wa Opium pamoja na viambata vyake vya kibaiolojia na Unga wa Cocaine ndivyo mashuhuri zaidi katika matumizi hayo.

Takwimu zifuatazo zinatoa mwangaza fulani juu ya athari ya dawa hizo za kulevya katika jamii:

- Jijini Washington, DC, nusu ya Waamerika weusi hivi sasa wamo jela au wamo katika orodha ya mahabusu wanaoachiwa huru kwa masharti ya kutorudia makosa. Zaidi ya asilimia tisini wana rekodi za kukamatwa-kamatwa. Hali ni hiyo hiyo kwa Waamerika weusi ndani ya miji ya Baltimore, New York, New Jersey, na Florida.
- Hadi mwaka 2000, takribani nusu ya Waamerika weusi walikuwa hatarini kwenda jela. Wengi wangekwenda magerezani kwa mashitaka ya kutumia dawa za kulevya. Wengi miongoni mwa wale waliokwenda jela wakaachiwa huru na kurudi tena katika jamii. Kwa vile walikuwa ni watu weusi wenye rekodi za kufungwa jela, ndio basi hawataajirika tena.
- Theluthi mbili ya wanafunzi wa kiume katika shule za ngazi ya juu walikuwa hatarini kufa, kuwa walemavu, au kufungwa jela kabla ya kusherehekea miaka thelathini ya umri wao. Wengi wao wangekwenda jela kwa mashitaka ya kutumia dawa za kulevya. Katika kila Waamerika weusi wanaokwenda shule, watatu huenda gerezani.

*'(Kushamiri kwa Vifungo gerezani,Wizara ya Sheria ya Marekani, 1980, na Kitabu cha Takwimu za Hukumu za Jinai.'Incarceration of Minority' Mradi wa Mahakama, Washington, DC, 1992. Matatizo ya Ajira ya Wafungwa walioachiwa huru,Wizara ya Sheria, Kitengo cha Magereza, 1992.'*

## Mkakati wa Clinton Dhidi ya Dawa za Kulevya

**Serikali mbalimbali zimetunga sheria za kudhibiti utumiaji, utengenezaji, usambazaji, umilikaji, uandikaji, uagizaji na usafirishaji wa 'Dawa Zilizozuiliwa'. Rais Bill Clinton, akiainisha mkakati wake dhidi ya Dawa za kulevya, alilitaka Bunge la Marekani kuidhinisha dola bilioni 15.1 katika mwaka wa fedha 1997 kwa ajili ya kufanikisha jitihada za kudhibiti dawa za kulevya.**

Jenerali mstaafu wa Jeshi la Marekani, Barry McCaffrey, Mkurugenzi wa Taifa wa Sera ya Kudhibiti Dawa za Kulevya, alisema, kulikuwa na takribani watumiaji milioni 11 wa dawa za kulevya nchini Marekani.

"Hii ni jitihada ya kipindi cha muongo mmoja kushughulikia kadhia hii tete", alisema Jenerali huyo alipozungumza na shirika la habari la NBC News katika kipindi cha "Meet the Press". Mkakati huu mpya unalenga kudhibiti dawa za kulevya miongoni mwa vijana na kutoa elimu mbali ya kutekeleza sheria na kudhibiti BIASHARA YA MAGENDO YA DAWA ZA KULEVYA, aliongeza Bw. McCaffrey. (Reuters: Jumatatu, Aprili 29, 1996)

Jumuiya ya Ahmadiyya inadai kuwa wao ndio 'Vinara wa Uislamu', kwamba ndio "vigezo" vya tabia njema ya Muislamu. Mwasisi wa Jumuiya ya Ahmadiyya, Mirza Ghulam Ahmad Qadiani, alidai kuwa yeye ni NABII, MAHDI, MASIHI ALIYEAHIDIWA, MWANA WA MUNGU, NA MUNGU na kadhalika.

Kwa hiyo, maisha yake yana athari ya moja kwa moja katika maisha ya Ahmadia au Makadiani wote ambao wanamtazama yeye kama KIONGOZI wao wa KIROHO na KIWILIWILI KIPYA cha MTUME MTUKUFU MUHAMMAD (saw).

Katika sehemu zifuatazo, nitafanya jitihada za kuyamulika maisha ya Mirza Ghulam Ahmad Qadiani kwa mnasaba wa KADHIA YA DAWA ZA KULEVYA na kuonesha baadhi ya vielelezo vya ushiriki wa AHMADIYYA/MAKADIANI katika USAFIRISHAJI WA DAWA ZA KULEVYA katika vipindi vya karibuni.

## Mirza Ghulam Ahmad Qadiani na **DAWA ZA KULEVYA+POMBE YA MKUYATI (TONIC WINE)**

"Nakumbuka mkasa mmoja, nao ni huu kwamba mimi nina kisukari kwa miaka kadhaa sasa. Nakojoa mara 15 hadi 20 kwa siku, na wakati mwingine, nakojoa mara mia-mia kwa siku. Kutokana na sukari kwenye damu, pia napata maambukizo ya mkojo, na kutokana na kukojoa kupita kiasi, nadhoofika sana. Jamaa yangu mmoja aliwahi kushauri kwamba Dawa za kulevya zinafaa kwa Wagonjwa wa sukari, hivyo, hakuna ubaya nikitumia kama tiba. Mimi nikamjibu: 'Ni jambo zuri sana wewe kunihurumia lakini nikijenga tabia ya kutumia Dawa za kulevya, nachelea watu wasije kukebehi MASIHI

WA KWANZA ALIKUWA CHA POMBE (MLEVI), NA WA PILI NAYE ALIKUWA TEJA'" (*Naseem Da'awat, Roohani Khazain vol.19 uks.434-435, by Mirza Ghulam Ahmad Qadiani)*

"DAWA ZA KULEVYA hutumika kwa wingi mno katika tiba kiasi kwamba Hazrat Masiih Muwuud (Mirza Ghulam Ahmad Qadiani) alikuwa akisema kwamba kwa mtazamo wa baadhi ya madaktari, Dawa za kulevya ni nusu ya tiba. Hivyo, kutumia Dawa za kulevya pamoja na tiba nyingine kama ponyo, na si kama ulevi, hakuna pingamizi lolote. Sote kati yetu, kwa kujua au bila kujua tumetumia Dawa za kulevya kwa wakati mmoja au mwingine...."

> Hazrat Masih Muwuud (Mirza Ghulam) alitengeneza dawa 'TIRYAQ-e-ILAHI' kwa maagizo kutoka kwa Mungu na moja ya vichanganyio vya dawa hiyo ilikuwa ni DAWA ZA KULEVYA ambapo Huzuur (Mirza Ghulam), baada ya kutia nyongeza ya Dawa za kulevya, akamnywesha Hazrat Khalifa Awwal (Hakiim Nurdiin, Mrithi wa kwanza wa Mirza Ghulam) kwa zaidi ya miezi 6, na akapumzika na kuendelea kutumia yeye mwenyewe wakati akisumbuliwa na maradhi mbalimbali."(*Article of Mian Mahmood Ahmad Saheb, Khalifa Qadian, Akhbar Al-Fazl vol.17 No.6 uk.2 Dated 19th July 1929)*
>
> Mmiliki wa Kiwanda cha uchapishaji anasema;
>
> "Pale Mirza alipokuja kwa mara ya kwanza katika kiwanda changu cha uchapishaji, alikaa kwenye kiti cha mto nami nikakaa kwenye kiti kingine, na akazungumzia kitabu. Nilipoyatazama macho yake ya kulewa-lewa, niliona huyu labda kanywa DAWA ZA KULEVYA kama ilivyo kawaida ya matajiri, lakini pale niliposikia uongeaji au usemaji wake, na nilipozitafakari makala za Brahiin-e-Ahmadiyya, nilishangazwa kuwa mbona hali ya mtumiaji wa Dawa za kulevya haiwi hivi, mtu kama huyu hawezi kuandika kitabu kama hiki. Kisha Hazrat Sahib akaondoka zake.....sasa nikajutia kosa langu la kwanza na nikatubia, na nikajua fika kuwa kumbe ule ni ULEVI WA ILIMU YA KIUNGU na si ulevi wa DAWA ZA KULEVYA kama nilivyodhani mwanzo. (*Statement of Qadiani Sahabi, Sheikh Noor Ahmad Saheb, Owner of Riyaz Hind Press, Al-Fazl Newspaper, Qadian, vol.34, No.194, dated 20th August 1940)*
>
> Mirza Bashiruddin naye anasema;
>
> "Utotoni mwangu, Mirza Ghulam alininywesha DAWA ZA KULEVYA kwa sababu ya kuumwa. Alininywesha kwa miezi sita mfululizo."(*Statement of Mirza Basheeruddin Mahmood, Khalifa Qadian, Minhaj-ul-Talibeen, p.74)*

"Ijumaa, Juni 28, majira ya asubuhi, Hazrat Khalifatul Masiih wa Pili, Mungu aitie nguvu mikono yake alichukuzana nami (Abdur Rahiim Dard), Dkt. Hashmarullah Sahib na Mian Nasir Ahmad Sahib kwenda kumtembelea Khwajah Kamaluddin (mshirika wa karibu wa Mirza Ghulam Ahmad Qadiani Sahib) wakati alipokuwa anaumwa. Khwajah Sahib akaanza kusimulia kadhia yake, ugonjwa alionao, na tiba aliyotumia. Alitaja kila kitu. Kumbe Khwaja Sahib naye siku hizi anatumia Dawa za kulevya. Alianza na dozi

ndogo (inayokaribia 1mg). Anakusudia kunywa dawa hizo kwa miezi sita ijayo ili mishipa yake ipate nguvu. (Diary Mian Mahmood Ahmad Saheb, Khalifa Qadian, Story

of Abdur Raheem Dar Qadiani, Al-Fazl Newspaper, Qadian, vol.17, No.2, dated 5th July 1929.

1929.

“Kipenzi changu  Hakiim Muhammad Hussein Saheb”

Assalaam Alaykum wa Rahmatullah wa Barakatuhu. Hivi sasa namtuma Mian Yah Mohammad. Nunua mwenyewe vitu vyote vinavyohitajika kununuliwa na nunua chupa moja ya POMBE YA MKUYATI kutoka kwanye Duka la Plommer. Lakini, na mimi nataka POMBE YA MKUYATI, zingatia jambo hili. Mapumzimko mema. Wassalaam.(signed) Mirza Ghulam Ahmad. *Letters of Imam towards Ghulam, p.5, Majmooa-e-Maktoobat Mirza Ghulam Ahmad towards Hakeem Muhammad Hussain Qureishi Saheb Qadiani, Owner of Rafeeq-us-Sehat Dispensary, Lahor).*

“Hivyo, katika mazingira hayo, kama Hazrat Masiih Muwuud (Mirza Ghulam) ametumia Barandi au Rum kwa ajili yake mwenyewe wakati alipokuwa anaumwa au kama amezitumia  kwa ajili ya wagonjwa wake, basi hiyo haikuwa kinyume na Sheria ya Kiislamu sembuse Pombe ya mkuyati ambayo ni tiba. Hata kama alikuwa ameinunua kwa mmoja wa watu wa familia yake au kwa jamaa yake ambaye alipona ugonjwa wa muda mrefu na kadhoofu, au hata kama aliiomba kwa ajili yake mwenyewe, na akaitumia, kulikuwa na ubaya gani? Alikuwa akisumbuliwa na magonjwa makali ya kudhoofu kiasi kwamba mikono na miguu yake ilikuwa ikipata baridi na akawa anatweta, huku akidhoofu. Mimi binafsi nimemuona akiwa katika hali hii. Ikiwa katika hali hiyo, kwa maelekezo ya madaktari, alitumia Pombe ya Mkuyati, basi hiyo iliendana sawasawa na Shariah (Sheria ya Kiislamu). Alikuwa akitumia siku nzima kuandika. Alikuwa akiswali usiku. Alikuwa anazidi kuzeeka. Hivyo, katika hali hiyo, iwapo alikunywa Pombe ya mkuyati kama ponyo, kuna tatizo gani?”
*(Statement of Dr. Basharat Ahmad Qadiani Lahori, Paigham-us-Sulh Newspaper, vol.23, No. 15, dated 4th March 1935; vol.23 No.65 dated 11th October 1935; mentioned in Qadiani Mazhab, pp. 168-169, 1995 Edition, by Prof. Mohammad Ilyas Burni)*

## 1985: Kasha Kubwa la Dawa za Kulevya lakutwa ndani ya Magunia ya Mchele Bandari ya Dubai

> "Imefahamika kuwa jitihada za kufanya biashara ya magendo ya mihadarati zimekwamishwa na Mamlaka za Dubai ambapo TANI MOJA ya mihadarati yenye thamani ya mamilioni ya dola, ilibambwa ndani ya kontena la Mchele. Kwa mujibu wa maelezo yaliyopatikana, mnamo Aprili 14, meli iitwayo Chitral ya Shirika la Meli la Pakistan, ikiwa na shehena ya mchele, iliwasili Dubai ikitokea Karachi ambapo mihadarati ilibambwa katika moja ya makontena yake. Mzigo huo ulitumwa kutoka Kampuni ya Usafirishaji wa Mchele Nje ya Nchi kwenda Kampuni moja ya Dubai.”(*Daily Jang, Karachi, 25th April 1985)*

Mnamo Aprili 14, 1984, meli ya mizigo ya Shirika la Meli la Pakistan iliwasili kwenye Bandari ya Dubai ikitokea Karachi. Ilikuwa na shehena ya MCHELE. Ndani ya Kontena mojawapo, ilikutwa tani moja ya DAWA ZA KULEVYA. Shehena hii ya mchele ilitumwa na Kampuni ya Usafirishaji wa Mchele Nje ya Nchi kwenda kampuni moja ya Dubai. Kulikuwa na ushahidi wa wazi kuwa MAKADIANI walihusika na Magendo haya ya DAWA ZA KULEVYA.

- Kwa miaka 12 Hamza bin Abdul Qadir Qadiani ndiye aliyekuwa Meneja Mkuu wa Kampuni ya Usafirishaji wa Mchele Nje ya Nchi ya Pakistan, hivyo, yeye ndiye aliyekuwa Msimamizi mkuu wa Kitengo kilichohusika na Upakiaji na Usafirishaji wa Mchele.
- S.K. Malik Qadiani ndiye aliyekuwa Msimamizi wa Kitengo cha Manunuzi cha Kampuni ya Usafirishaji wa Mchele ya Pakistan
- **S. Abdul Ghani Qadiani ndiye aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Fedha ya Kampuni ya Usafirishaji wa Mchele Nje ya Pakistan. Kama kawaida hakuna kilichoweza kufanyika dhidi ya 'masangara' hawa ilihali dagaa waliadhibiwa.**
- "Makadiani Wanne kutoka Rabwa hivi karibuni walihukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela pamoja na kazi ngumu kule Abu Dhabi kwa kosa la KUFANYA MAGENDO na KUUZA DAWA ZA KULEVYA ndani ya nchi hiyo." (*Daily Jang Newspaper, Quetta, dated 27th May 1985*) *Khatme Nabuwwat, Weekly Magazine, No. 45 10-16 May 1985.*

# 1996: Dawa za Kulevya zabambwa ndani yaMifuko ya mchele iliyosafirishwa kwenda Birmingham, Uingereza

**BIASHARA YA DAWA ZA KULEVYA CHINI YA MWAMVULI WA WAZIRI WA MAMBO YA NJE**

**Dawa za kulevya zilibambwa ndani ya Mifuko ya Mchele iliyokuwa mbioni kusafirishwa kwenda Uingereza na Kampuni iliyomilikiwa na nduguye Sardar Asiif Ahmad Ali**

**Mnamo Aprili 25, 1996, Afisa Ukaguzi wa Idara ya Forodha, Kitengo cha Usafirishaji wa Bidhaa nje ya nchi alikuwa akitimiza wajibu wake wa kila siku kwenye Shehena Na. TR-5, Karachi East Wharf, Kemari. Wakati akifanya kazi yake, Nyaraka za Kusafirishia mzigo za Kontena Na. FLXU-9-201323 zikamfikia pamoja na Ankara ya Meli Na. 22796, ya tarehe 23 Aprili 1996. Kwa mujibu wa nyaraka hizo, kontena lilisheheni mifuko 950 ya mchele wa Basamati uliokuwa**

**ukipelekwa kwa Bw. Wippolyte wa** Ebony Food International, 55 Diagonal Road, Acocks Green, Birmingham B27 6ST UK.

Wakati wa ukaguzi, pale alipokuwa akipapasa-papasa moja ya mifuko ya chini kabisa, mfuko huo ukapasuka ambapo Afisa huyo Mkaguzi alishindwa kuamini macho yake pale alipoona kete za Dawa za kulevya zikianza kumwagika. Jumla ya kilo 119 za dawa za kulevya zilifungwa kiufundi sana na kuchanganywa na mifuko ya mchele kiasi kwamba katika kila mifuko 150 ya mchele, kulikuwa na kilo moja ya mfuko wa Dawa za kulevya. Mifuko hiyo ilipuliziwa uturi wa kuzuia mbwa wa kunusa wa Forodha wasiweze kuigundua harufu ya dawa hizo.

Alama zilizowekwa juu ya mifuko ya mchele na zile zilizowekwa juu ya mifuko ya dawa za kulevya zote zilikuwa na namba za mfuatano zilizolingana jambo ambalo lilionesha kuwa mzigo wa magendo kutoka Lahore kwenda Birmingham ni uleule wa mchele, na hivyo walikuwa na uwezo wa kuutenganisha kama watakavyo bila hofu ya kukamatwa.

Mwanahabari mmoja wa Masuala ya biashara katika gazeti la Kila siku la Kiwudu 'Nawa-e-Waqt' alifika mara moja na kupiga picha shehena nzima. Kwa mujibu wa taarifa yake ambayo aliifikisha kwenye ofisi ya gazeti lake hilo la kila siku, kilo 210 za dawa za kulevya zilifichuliwa na Afisa Makusanyo mwandamizi wa Forodha ndani ya mifuko ya mchele.

Forodha ikawakamata watu watatu akiwemo wakala wa upakuzi na uondoshaji wa mizigo Bandarini. Afisa huyo alizitaarifu mamlaka kuwa Kontena hilo lililofungwa lilitoka katika kampuni ya Ukoboaji wa mchele, Indus Rice Mill ambayo inamilikiwa na Sardar Haruun Ahmad, nduguye Waziri wa Shirikisho, ambaye alikataa nduguye kuhusika na Magendo ya Dawa za Kulevya, na kwamba aachiwe kwa dhamana. Hata hivyo, alinyimwa dhamana. Kwa upande mwingine, shinikizo likaielemea Forodha kwamba inyamaze kimya kuhusiana na kashfa hiyo.

Ripoti hiyo ilikuwa sahihi katika kila kipengele isipokuwa tu kwamba siku ya kwanza, Mamlaka za Forodha zilitangaza kuwa uzito wa dawa hizo za kulevya ulikuwa ni kilo 210, lakini siku iliyofuata pale F.I.R iliporekodiwa, kiasi kilikuwa ni kilo 119.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, punde mzigo wa dawa za kulevya ulipozuiliwa, Wathamini wa Forodha walizitaarifu mamlaka za juu zaidi. Kwa upande mwingine waliohusika na kashfa hiyo hawakuwa kundi dogo. Ilikuwa ni kampuni ya Ukoboaji Mchele ya nduguye Sardar Asiif Ahmad Ali, Waziri wa Mambo ya Nje na ambaye ni mwanachama mzito wa chama cha Chatta People Party, Muungano wa PDF wa Duru za utawala za Pakistan.

Hivyo, ofisi za Indus Rice Mill zikafungwa na Viongozi wakatoweka. Kwa siku nne zilizofuata hakukuwa na dalili yoyote ya kuwepo mtu anayehusika na kiwanda cha Indus Rice Mill. Katika kipindi hiki, Sardar Haruun Ahmad na nduguye, Sardar Asiif Ahmad, Waziri wa Mambo ya Nje wakatumia ushawishi wao serikalini kuwalinda wasikamatwe na wala hati zozote za kikazi zisitolewe dhidi yao. Badala yake, walijitahidi kulifunika suala hilo kwa kutumia ushawishi wao ambapo jitihada hizo bado zinaendelea.

Sardar Asiif Ahmad na Jamaa zake "Wazito" walipania mno kuzidhibiti mamlaka za Forodha ili mawakala wao waendelee kuzuia gazeti la Nawa-e-Waqt lisichapishe habari hii siku iliyofuata. Licha ya ahadi zao nono, kadhia nzima ikaripotiwa gazetini Aprili 26

Katika kuwahi kuepusha fedheha na usumbufu utokanao na uhalifu huo, mtandao mzima wa serikali na msonge wake mjini Islamabad ukaingia kazini. Mwanzo lawama zote zilielekezwa kwa wakala wa Uondoshaji wa mizigo Bandarini ambaye alitiwa mbaroni. Hata hivyo, punde tu kampuni yake iliposikia mkasa huo, ikachukua hatua na kumfanya aachiwe huru.

Baada ya kushindikana kwa jitihada hizo, shauri likahamishiwa katika Mamlaka za Uchunguzi za Shirikisho ambapo lawama zikahamishiwa kampuni ya MizigoTCS Courier Service ambayo ndiyo iliyohamisha kontena kutoka Lahore kwenda Karachi. Meneja wake wa Mkoa, Shafqat Ali akakamatwa kwa mashitaka kuwa wakala wake ndiye aliyeweka dawa za kulevya wakati akisafirisha kontena hilo kutoka Lahore kwenda Karachi.

Habari zikatolewa kwenye vyombo vya habari kwamba Mamlaka za Forodha zimeanza kuchunguza kuhusika kwa kampuni hiyo ya mizigo na magendo ya dawa za kulevya. Nukta muhimu kuzingatiwa ilikuwa ni kwamba katika F.I.R, jina la Msafirishaji, Indus Valley Rice Mill, halikuwemo kabisa.

Kwa matakwa ya mamlaka za juu, mamlaka ya uchunguzi ya shirikisho, F.I.A, ikaonesha dosari katika Jalada la FIR ili kwa msingi huo mahakama itilie shaka nia za mamlaka. Hivyo, yule wakala wa kampuni ya mizigo akaachiwa.

Kwa hiyo, Mamlaka za Forodha zikashinikizwa kufungua jalada la FIR alasiri ya Aprili 26 ambapo mahali pa mshitakiwa wa kwanza, bila kuandikwa jina wala anuani ya mtu yoyote yule, akatajwa tu 'Muajiriwa wa Msafirishaji'.

Kwa maneno mengine, kwa jeuri ya kupuuza sheria na haki, badala ya kuandika jina la mshitakiwa halisi na mmiliki halisi wa Kampuni ya Usafirishaji, ikaamuliwa kumtafuta mbuzi wa kafara (mtu wa kumsingizia) ambaye ni mmoja wa waajiriwa. Mahali pa pili kukawa na jina la Bw. Shafqat Ali wa Kampuni ya Mizigo, na mahali pa tatu alikuwa Bw. Hippolyte, na mahali pa mwisho, paliandikwa, 'NA WENGINE'.

Ufanisi na uadilifu wa mamlaka za Upelelezi, FIA, za Karachi haukupendwa mjini Islamabad, na hivyo, kesi ikahamishiwa kwenye mamlaka za upelelezi za Lahore ambako pia kazi yao ya uchunguza haikuonekana kuwaridhisha kabisa wahusika, hivyo, kesi ikahamishiwa kwenye Kitengo Maalum cha Upelelezi chini ya usimamizi wa moja kwa moja wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka za Upelelezi (FIA), mjini Islamabad.

Sasa mchezo mzima ukachezwa mjini Islamabad ambako ndiko waliko wahusika wenye ushawishi. Ni muhimu kuzingatia kuwa idadi kubwa ya waajiriwa wa kampuni ya Indus Valley Rice Mill ni ndugu wa nasaba wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje. Ugunduzi mwingine muhimu uliofanywa na Mamlaka za Upelelezi za Lahore ulikuwa ni kwamba mifuko kama hiyo hiyo ya mchele iliyochanganywa na dawa za kulevya zilizofungwa kitaalamu kwenye mifuko pia ilikamatwa katika Kampuni ya Ukoboaji ya Lahore.

## Mkutano wa Bw. Binyamiin na Waandishi wa Habari

**Sikukuu ya Juma zima ya Idd-ul-Adha iliwapa afueni wahusika. Mnamo Mei 4, Bw. Bw. Bin Yamiin Rizvi, Katibu wa Habari wa Jumuiya ya Kiislamu alifanya mkutano na waandishi wa Habari mjini Lahore na akamshutumu Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Sardar Asiif Ahmad Ali, kwa kuhusika na MAGENDO YA DAWA ZA KULEVYA.**

**Aidha aliishutumu serikali kwa kufanya hila ya kuifunika kashfa hiyo nzima. Akielezea kutoridhishwa kwake na ufuatiliaji wa serikali, yeye amemuomba Jenerali Jehangir Karamat Qadiani kuchunguza kadhia hiyo kwa kutumia Kitengo cha Ujasusi cha jeshi, na kuipeleka kesi hiyo Mahakama Kuu.**

**Alisema kuwa Sardar Asiif Ahmad ndiye mmiliki wa kampuni ya Indus Valley Rice Mill ambaye ana ofisi yake kule Chak Malik, Barabara ya Raiwind. Mtendaji wake Mkuu ni ndugu yake, Sardar Haruun Ahmad. Alimshutumu Asif Ali Zardari, mume wa aliyekuwa Waziri Mkuu wa Pakistan, Benaziir Bhutto, kwa kuziamrisha mamlaka kuteketeza dawa hizo za kulevya na kuifunika kadhi nzima, mbali na mambo mengine.**

**Bwa Bin Yamiin akasema kuwa Mwenyezi Mungu aikinge nchi ambayo Waziri wake wa Mambo ya Nje kawa mwanamtandao wa Mafia katika Dawa za Kulevya. Alishutumu kuwa Sardar Asiif ndiye Mkuu Mtandao wa Dawa za Kulevya wa Mafia katika nchi za Uingereza na Amerika.**

**Sardar Asiif Ahmad, huko nyuma, aliwahi kufukuzwa katika Baraza la Mawaziri la Nawaz Shariif kwa kosa la kutoa siri fulani na kuipa serikali ya India ambapo kesi ilikuwa ikiandaliwa dhidi yake pale serikali ya Nawaz Sharrif ilipoondolewa madarakani.**

**Aliongeza kuwa hakuna chochote ambacho kingetarajiwa kutoka serikali ya Banaziir Bhutto kuhusiana na suala hili kwa sababu huyu ni Waziri Mkuu ambaye mbunge mmojawapo wa chama chake, Munawwar Manoj ni Mwanamagendo wa Dawa za kulevya aliyeachiwa huru kutoka rumande licha ya kuhusika na Magendo ya Dawa za Kulevya, na kukamatwa na Bodi ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya, na kisha bado eti akamfanya mtu huyo huyo kuwa Mkuu wa Bodi ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Bw. Bin Yamiin amemuomba Waziri wa Mambo ya Ndani kuifanyia uchunguzi kadhia nzima kwa kuwatumia watu madhubuti.**

Kauli ya Sardar Asiif'/Haruun:

Mamlaka za Upelelezi za Lahore zilitoa taarifa ya kufafanua nafasi ya wamiliki wa Kampuni ya Mill. Yasemekana kuwa Sardar Haruun Ahmad ametoa taarifa kuwa baadhi ya wafanyabiashara za magendo wanajaribu kufanya magendo ya dawa za kulevya katika mchele ulionunuliwa kutoka kampuni yake ya mchele. Amemuomba Waziri wa Mambo ya Ndani kuchunguza jambo hilo.

**Bw. Gohar Ayub Khan:**

Naibu Kiongozi wa Upinzani alitoa taarifa mnamo Mei 6. Katika taarifa hiyo, amesema kuwa namna zinafofanyika jitihada za kuonesha Sardar Asiif Ahmad Ali hana hatia, yenyewe tu inafanya kadhia nzima itiliwe shaka kabisa.

Ni tuhuma nzito dhidi ya Sardar Asiif, na kama Mahakama haitasikiliza kadhia nzima na kumwacha huru kwa utaratibu unaokubalika, basi machoni mwa Taifa na Sheria, atabaki kuwa mtuhumiwa.

Akashauri kuwa lazima aheshimu nafasi yake, na aheshimu unyeti na uzito wa Wadhifa wake, na kama hana uadilifu wa kujiuzulu wadhifa alionao, basi angalau aende likizo katika kipindi chote ambacho Mahakama inashughulikia hukumu yake.

Hakuna Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi yoyote yenye mamlaka inayojitawala ambaye angependa kufanya mazungumzo na Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi yetu ambaye ni mshitakiwa, na endapo atang'ang'ania madaraka yake, ndio basi hataweza kutimiza wajibu wowote kwa maslahi ya nchi yake, badala yake atakuwa chanzo cha kero kwa Taifa zima na kwa Wizara yake.(Takbeer, International Urdu Weekly, No. 20 dated 16th May, 1996; Nasir Mahmuud)

(Tafadhali: Ni muhimu kuzingatia kuwa baada ya ripoti chache za mwanzo, kumekuwa na giza totoro katika habari inayohusu kadhia hii)

## Kuhusika kwa Makadiani:

Bw. Manzuur Ilahi Malik Awan wa Gazeti la Kila wiki la Khatmi Nabuwwat ameripoti kuwa Bw. Sardar Asiif Ahmad na Bw. Nasiirulla Baber, Waziri wa Mambo ya Ndani wa Pakistan ni AHMADIA (MAKADIANI). Utafiti mwingine ambao haujachapishwa unabainisha kuwa kati ya nyadhifa tatu za ngazi ya juu katika Kada za Utumishi wa Ndani ya nchi, Nje ya Nchi na Jeshini nchini Pakistan, mbili zinashikiliwa na Makadiani/Ahmadia/Lahoria.

Pakistan ni mojawapo ya vichochoro vya magendo ya dawa za kulevya kuelekea Ulimwengu wa Magharibi. Kukiwa na MAKADIANI/AHMADIYA wenye ushawishi namna hiyo, pamoja na washirika wao katika mamlaka za utawala za Pakistan, ni dhahiri, kesi hii inafichua yale ya juu-juu tu huku mengi yakibaki chini.

## Mwisho

Tangu mwaka 1980, kumekuwa na uhamiaji wa wafuasi wa Jumuiya ya Ahmadiya katika maeneo mbalimbali ya nchi za Ulaya na Amerika. Kwa sababu ya propaganda za Makadiani/ Ahmadia kuhusu kile kinachoitwa 'Manyanyaso ya Ahmadiyya nchini Pakistan', Nchi za Magharibi zinawapa hifadhi kwa misingi ya kibinadamu. Ni bahati mbaya ilioje kwamba m-miminiko wa Dawa za Kulevya kutoka Mashariki kwenda Magharibi nao umeongezeka sawia katika kipindi hicho hicho.

Jumuiya ya Ahmadiyya inatumia kiasi kikubwa cha fedha katika kusambaza itikadi zake potofu kwa jina la Uislamu. Baadhi ya miradi yake ni

- .Kuchapisha na kusambaza Qur'an Tukufu katika lugha 140;
- Kuchapisha majarida ya wiki na mwezi katika lugha 120;
- Kuchapisha maandiko mengine 100 ya propaganda;
- Kuendesha Matangazo ya Saa 24 ya Lugha kadhaa Dunia Nzima Kupitia Televisheni ya Ahmadiyya;
- Kuendesha Matangazo ya Kila siku Kwa Kiurdu, Kirusi, Kiingereza na Kibangladeshi;
- Kuendesha Mahubiri ya nyumba kwa nyumba, (na ya mitaani) katika miji yote mikubwa ya nchi 120.
- Kuendesha Hospitali/kliniki, Vituo vya Kijamii, shule n.k katika nchi kadhaa

Makadiani/Ahmadia wa kawaida huzugwa na kuamini kuwa mchango utokanao na kipato chao kigumu ndio unaoendesha miradi hiyo. Wanakataa kata kata kuwa Nguvu za Maadui wa Uislamu ndizo zinazochangia harakati za Ahmadiyya.

Ni ukweli unaofahamika vema kuwa baadhi ya watu hujiingiza katika Magendo ya Dawa za Kulevya ili kupata fedha za haraka-haraka na kuwa mabilionea kwa usiku mmoja tu. Katika kadhia zinazofichuliwa, zipo nyingine ambazo hazikamatwi.

Tunaziomba mamlaka za udhibiti wa Dawa za Kulevya katika nchi za Ulaya, Marekani na sehemu nyingine ulimwenguni zitazame upya mkondo mzima kwa kuzingatia taarifa za hapo juu na zijaribu kuchunguza uhusiano baina ya Magendo ya Dawa za Kulevya na Ongezeko kubwa la Uhamiaji wa Makadiani/Ahmadia katika nchi za Magharibi.